**Masomo ya Biblia**

**kwa ajili ya**

**KANISA LA ELOHIM (COG)**

**Siku Ya Saba (7th day)**

---

**Robo Ya Nne**

**2016**

---

**KWA AJILI YA**

**Oktoba, Novemba, Desemba.**

**Kutumika na Biblia**

---

**Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

---

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**

**Jerusalem - Israel**

-----------------------------------------------------

**Somo La Tarehe Oktoba 1, 2016.**

**KUTOTII KWA SAULI NA KUKATALIWA KWAKE**

**Somo Kuu: 1 Samweli 15:1-23**

**Fungu la Kukariri: 1 Samweli 15:23.**

1. Ni kosa lipi Sauli alitenda kwanza baada ya kufanywa mfalme? 1 Samweli 13:5-9.
2. Baada ya dhabihu kutolewa, ni nani ambaye alionekana? 1 Samweli 13:10.
3. Swali la Samweli kwa Sauli lilikuwa lipi? Jibu la Sauli lilikuwa lipi? 1 Samweli 13:11, 12.
4. Samweli alitoa tangazo gani? 1 Samweli 13:13.

5. Je, ni mtu wa aina gani angechukua ufalme baada ya Sauli? 1 Samweli 13:14.

   **Dokezo**: Hatua hii mbaya ya kwanza ilihathiri hatima yake Sauli milele (ingawa alipewa muda wa kujichunguza mwenyewe na kuamua jinsi mwenendo wake wa baadaye utakuwa). Kutotii makusudi mara moja tu kunatosha muhuri wa adhabu yetu, kwani hutuchoma dhamiri zetu na kufanya kutenda dhambi nyingine kuwe rahisi sana.

6. Baada ya muda, amri gani ambayo Samweli alitoa kwake Sauli? 1 Samweli 15:1-3.
7. Ni kiasi gani cha amri hii Sauli alitii? 1 Samweli 15:7-9.
8. Samweli alipata ufunuo upi? 1 Samweli 15:10, 11.
9. Sauli alisema nini wakati walikutana na Samweli? 1 Samweli 15:12, 13.
10. Ni nini iliothihirisha uongo katika taarifa yake Sauli? Kisingizio chake kilikuwa kipi? 1 Samweli 15:14, 15, 24.
11. Dhambi, uasi na ukaidi inalinganishwa na nini? 1 Samweli 15:23.
12. Je, Samweli alimtembelea Sauli tena baada ya Sauli kutenda dhambi kwa makusudi? 1 Samweli 15:34, 35.

******************************

**Somo La Tarehe Oktoba 8, 2016.**

**KIBURI**

**Somo Kuu: Danieli 4.**

**Fungu La Kukariri: Mithali 16:18.**

1. Katika Orodha ndefu ya mambo ambayo Bwana anachukia, ni jambo lipi la kwanza lililotajwa? Mithali 6:16-19.
2. Kwa nini waovu hawatamtafuta Baba wa Mbinguni? Zaburi 10:4.
3. Kiburi cha mtu kitamfaidi nini? Mithali 29:23.
4. Ni nini imetajwa katika Mithali 16:18, ambayo itakuja kabla ya uharibifu?
5. Ni nini ilikuwa sababu ya Ibilisi kuanguka? Isaya 14:12-15.
6. Ni cheo kipi Hamani alishikilia kwa wakati mmoja katika ufalme wa Uajemi na Umedi? Esta 5:7-12.
7. Kwa hasira yake dhidi ya Mordekai alifanya nini? Esta 5:13, 14.
8. Jinsi gani Hamani alikutana na kifo chake? Esta 7:10.

   **Dokezo**: Huyu ni mtu ambaye alishikilia nafasi ya juu sana katika maisha yake lakini akawa wa kuinuliwa kupitia kiburi chake. Alikutana na hatima yake chungu, kuwa alinyongwa juu ya mti aliomwekea tayari mtu aliyemchukia.

9. Ni nini ilitendeka kwa mfalme Nebukadreza kwa sababu ya kiburi? Danieli 4:30-33.
10. Je, ni somo lipi kubwa huyu mfalme alijifunza kupitia njia ngumu? Danieli 4:34-37.
11. Kiburi huwa chatoka wapi? 1 Yohana 2:16.

******************************

**Somo La Tarehe Oktoba 15, 2016.**

**KUSAMEHEANA**

**Somo Kuu: Matthew 18.**

**Fungu La Kukariri: Mathayo 6:15.**

1. Ni jambo lipi la muhimu twafaa kufanya ili kupokea msamaha wa dhambi zetu? Marko 11:25.
2. Je, Elohim atawasamehe wale huwa hawasamehi wenzao? Mathayo 6:15; Marko11:26; Mathayo 18:35.

   **Dokezo**: Elohim aridhiki na huduma ya mdomo tu. Ni sharti tusameheane kutoka moyoni, na tunapofanya hivyo tutasahau pia, na tutakoma kukaa kwa dhambi ambayo ishasemehewa. Baadhi ya wengine wakidai wamesameheana husema: naweza kusamehe lakini siwezi kusahau yao, wao huendelea kuwa na kinyongo.

3. Ni katika hali gani lazima nyoyo zetu zinafaa kuwa ili kwamba tupate kupokea msamaha? Mathayo 6:12.
4. Je, Elohim alikataza watu kuwa na kinyongo? Mambo ya Walawi 19:18.
5. Je, agano jipya inasema nini kuhusu kuwa na kinyongo? Yakobo 5:9; Mathayo 6:12-14

   **Dokezo**: Wivu, dhambi iliyotawala kwa miaka hata sasa kama ilivyokuwa nyakati za ndugu wa Yusufu, wakawa na wivu kwake yeye kwa sababu ya upendo na ukarimu wa ziada alioupata kutoka kwa wazazi wake, na pia kwa sababu Elohim alionyesha neema kwake na alimpa yeye ndoto kuhusu mambo ambayo yangekuja kupita karibuni, kwa hayo walimtesa na kumuuza kwa wageni ili awe mtumwa.

6. Jinsi gani Yusufu mtu wa Elohim aliwasamehe ndugu zake? Mwanzo 45:15.
7. Katika kukabiliana na kukosea, ni hisia gani zinafaa kutuamilisha? Mathayo 18:33.
8. Wale ambao watashindwa kuonyesha rehema kwa wengine watatarajia nini? Yakobo 2:13.
9. Ni nini ilitokea kwa mtumishi ambaye alikuwa na deni kubwa? Mathayo 18:23-27.
10. Baadaye, wakati mtu mmoja alikuja ambaye alidaiwa na huyu mtu deni ndogo tu, alipokea rehema gani? Mathayo 18:28-30.
11. Huyu mtumishi ambaye hakuonyesha rehema alipokea nini kutoka kwa Bwana wake? Mathayo18:32-35.
12. Ni kwa ajili ya nani haya yote yaliandikwa? 1 Wakorintho 10:11; Warumi 15:14; 2 Timotheo 3:16, 17.

*******************************

**Somo La Tarehe Oktoba 22, 2016.**

**MWANAKONDOO WA ELOHIM - MKUU NA BWANA**

**Somo Kuu: Yohana 1:29-41.**

**Fungu La Kukariri: Yohana 13:13.**

1. Ni kwa madhumuni gani muhimu Masihi Yahshua alitumwa ulimwenguni? Marko 10:45.
2. Ni nani peke yake alihitimu kama mbadala wa kila mwenye dhambi? Yohana 1:29.
3. Ni ukweli upi wa milele Yahshua alieleza kwa niaba ya kila mtoto? Mathayo 18:14.
4. Yahshua alisema nini kuhusu yeye mwenyewe? Yohana 13:13.
5. Ni nini huja kwa kila mmoja wetu ambaye anaishi katika dunia hii ya sasa? Yohana1:9.
6. Kabla Masihi ajapaa, Yeye aliwamuru wafanye nini wafuasi wake? Mathayo 28: 19.
7. Je, wafuasi wake watafundisha nini? Mathayo 28: 20.

   **Dokezo**: Biblia peke yake inafaa iwe mwongozo wetu na sheria katika yote twafundisha. WaMasihi wa kweli watakuwa makini kutoongeza chochote juu ya imani yao ambayo haikupatikana kwa mafundisho au mienendo ya Yahshua. Wakati ukweli huu huimarishwa, njia yetu inakuwa wazi.

8. Jinsi gani tutakavyoenda kama tutaamini kikamilifu na kuweka imani yetu katika Yahshua? 1 Yohana 2:6.
9. Jinsi gani imani yetu katika Yahshua itajulikana? Warumi 6:17, 18; Waefeso 2:10.
10. Ni ushahidi gani Yakobo anatumia kuonyesha kwamba "imani" huleta "matendo"? Yakobo 2:18, 20-23.

*******************************

**Somo La Tarehe Oktoba 29, 2016.**

**KUFUFUKA**

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:1-58**

**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:22.**

1. Je, kila mtu atafufuliwa? Yohana 5:28, 29.
2. Wenye haki watafufuliwa wakati upi ili waingie katika uzima wa milele? 1 Wakorintho 15:22, 23; Ufunuo 20:41 Wathesonike 4:16.
3. Ni nini kitatokea kwa Watakatifu ambao watakuwa hai wakati Yahshua atafunuliwa? 1 Wathesonike 4:17; 1 Wakorintho 15:51-53.
4. Ni wapi ambapo Watakatifu waliofufuka watakaa na kazi yao itakuwa ipi wakati wa miaka elfu moja? Ufunuo 5:10; Danieli 7:27; Luka 19:15-19.

   **Dokezo**: Ni Baraka za ajabu zawangoja waumini wote katika Masihi Yahshua! Wote waliokufa katika Bwana watafanywa kuwa hai wakati wakufunuliwa kwake Yahshua, wakati Watakatifu walio hai watabadilishwa mili yao katika dakika moja, kufumba na kufumbua, na wataishi na kutawala pamoja na Masihi miaka elfu. Wakati huu Yahshua atakuwa akitawala katika kiti cha enzi cha Daudi. Luka 1:32; Isaya 24:23.

5. Walio wafu waovu watakuwa wapi katika wakati huu wa miaka elfu? Ufunuo 20:5, 6.

6. Wale waovu watawahi kufufuliwa? Yohana 5:28, 29.
7. Ni kwa madhumuni gani wale waovu wataletwa mbele? Ayubu 21:30; 2 Petero 2:9.
8. Wakati waovu watafufuliwa, ni wapi ambapo ni lazima watafika? Ufunuo 20:11, 12.

   **Dokezo**: Hukumu ni kwa ajili ya waovu, kwani wenye haki walienda hukumuni wakati walikiri dhambi zao, walizaliwa tena na wakawa watiifu kwa maneno ya Bwana; kwa hivyo walipita kutoka mautini kuingia uzimani na wakawa washiriki wa familia ya Elohim. 1 Timotheo 5:24; Yohana Mtakatifu 5:24.

9. Hatima ya waovu itakuwa ipi? Ufunuo 20:13. 15; 21:8.

*******************************

**Somo La Tarehe Novemba 5, 2016.**

**SHERIA NA INJILI**

**Somo Kuu: Yakobo 2:1-16**

**Fungu La Kukariri: Yakobo 2:23, 24.**

1. Kwa ajili ya jambo jema kwa mtu, katika mwanzo, Elohim alimpa nini? Mwanzo 2:16, 17.

   **Dokezo**: Hakuwezi kuwa na serikali kamilifu iwe imetengenezwa na watu au ya kidini. Kila serikali nzuri hutoa sheria kwa manufaa ya wananchi wake. Wale wanaopinga sheria ya Elohim huonyesha ya kwamba hawana upendo kwa mtu na heshima kwa Elohim.

2. Ni swali lipi mmoja wa waandishi aliuliza Yahshua? Marko 12:28.
3. Jinsi gani Yahshua alimjibu? Marko 12:29-31.
4. Ni wapi ambapo tunapata muhtasari wa kina zaidi wa kweli hizi? Kutoka 20:1-17
5. Jinsi gani Paulo aliuonyesha ukweli? Warumi 13:8-10, 14.
6. Ni nini ilizingatiwa na ni sheria gani iliyotumika kwa ulimwengu wa mataifa yasiyokuwa na sheria? Warumi 2:14-16.
7. Je, kuvunja sheria kumesemekana kuwa nini? Warumi 13:2.

   **Dokezo**: Sheria haifanyi watu wenye dhambi. Spidomita kwenye gari haisababishi mtu kuendesha kwa kasi zaidi ya kipimo kilichowekwa. Inaonyesha tu wakati mtu amekiuka hukumu nzuri au sheria zilizowekwa.

8. Ni nafsi ngapi zinazookolewa kwa sheria pekee? Warumi 8:3.
9. Wakati sheria inaonyesha dhambi, ni nini injili hutimiza? Warumi 1:16.
10. Tukishapokea injili, uhusiano wetu mpya na Elohim utakuwa upi? Yohana 1:12.
11. Ni kwenye hali gani wokovu utapeanwa? Waebrania 5:7-9.
12. Jinsi gani Yakobo anaonyesha amri kumi? Yakobo 2:8-12.
13. Ni sherehe gani inaunganisha sheria na injili? Warumi 6:4.
14. Ni hitimisho gani ya kutia fora Yakobo anatoa? Yakobo 2:14, 26.

*******************************

**Somo La Tarehe 12 Novemba 2016.**

**UJUMBE WA UPATANISHO**

**Somo Kuu: 2 Wakorintho sura ya 5.**

**Fungu La Kukariri: 2 Wakorintho 5:19.**

1. Ni kupitia nani twapata upatanisho? 2 Wakorintho 5:18.
2. Ni nini tumekabidhiwa? 2 Wakorintho 5:19.
3. Ni nini hufanya upatanisho kuwezekana? Matendo ya Mitume 2:38.

   **Dokezo**: Wengi wanaona kuwa ni vigumu kuishi maisha ya uMasihi. Sababu ni, ingawa wamepatanishwa na dhambi zao kusamehewa, akili zao hazijabadilishwa kwa mambo ya kiroho. Upendo kwa raha za ulimwengu na mitindo yake bado inawashika na kuwazuia.

4. Je, wahudumu wa Masihi wameitwaaje katika 2 Wakorintho 5:20?
5. Je, karama ya Elohim ni nini? Warumi 6:23.
6. Tunapaswa kufanya nini baada ya kupatanishwa na Elohim? Warumi 12:1.
7. Ni kwa namna gani hatufai kujifuatisha ? Mstari wa 2 (Sehemu ya kwanza).
8. Ni kwa namna gani tunapaswa kubadilishwa? Mstari wa 2 (sehemu ya mwisho).
9. Je, ni aina gani ya ahadi hutokana na upatanisho? 2 Petro 1:4.
10. Ni nini inapea uhai neno la Elohim? Yohana 6: 63.
11. Mtu aliyepatanishwa anapaswa kuishi kwa? Mathayo 4:4.
12. Je, maandiko yana uwezo wa kufanya nini? 2 Timotheo 3:15.

*******************************

**Somo La Tarehe 19 Novemba 2016.**

**UKAMILIFU KATIKA MWENDO WA UZIMA**

**Somo Kuu: Wafilipi 3.**

**Fungu La Kukariri: Wafilipi 3:14.**

1. Ni nini ilikuwa kiwango ambacho Nuhu alifikia katika siku alizoishi? Mwanzo 6:8, 9.
2. Ni kiwango gani Elohim alihitaji kutoka kwa Ibrahimu? Mwanzo 17:1.
3. Ni nini inayoonyesha kwamba Henoko aliufikia ukamilifu? Mwanzo 5:22-25; Waebrania 11:5.
4. Je, agano jipya inasema nini kuhusu Zakaria na Elisabeti? Luka 1:5, 6.
5. Ni katika hali gani Elohim aliahidi kuimarisha Sulemani juu ya kiti cha enzi cha mfalme Daudi? 1 Wafalme 9:3-5.
6. Nini  kilichosemwa kuhusu wale walioufikia ukamilifu? Zaburi 37: 37..

7. Ni maagizo yapi yaliotolewa kwa Israeli kwa ajili ya huu ufikiwaji? Kumbukumbu la Torati 18:9-13.
8. Ni nini kilichosemwa kuhusu mataifa ya Kanaani? Kumbukumbu la Torati 18:14.

   **Dokezo**: Katika pembeni mwa Bibilia inaonyesha "kamili" kama "unyofu" au "uaminifu". Mtu mkamilifu ni yule aliyemwaminifu na hana nia ya kufanya makosa.

9. Ni nani ambaye Bwana wetu Yahshua alimweka kama mfano kwetu wa ukamilifu? Mathayo 5:48.
10. Ni nini ambayo ni lazima matajiri wanafaa kufanya ili waweze kuufikia ukamilifu? Mathayo 19:16-21.
11. Jinsi gani tajiri yule alijibu kuhusu hitaji hili? Mathayo 19:22.
12. Katika fumbo fulani, ni kiasi gani tunatakiwa kuuza ili kupokea wokovu? Mathayo 13:45, 46.

    **Dokezo**: Ubinafsi ndio kikwazo pekee katika lengo letu la kuufikia ukamilifu. Utajiri huzuia matajiri. Ni nini huzuia maskini? Je, huwa twauza vyote? Baadhi yetu huweka hazina ya uovu, wivu, hasira, na udanganyifu katika nafsi zetu na kukataa kuviuza vyote ili kununua lulu ya thamani kuu, lulu ambayo ni Masihi.

******************************

**Somo La Tarehe Novemba 26, 2016.**

**IMANI KATIKA NENO LA ELOHIM**

**Somo Kuu: Warumi 4**

**Fungu La Kukariri: Warumi 4:3**

1. Taja mambo manne imani ilitimiza katika Waebrania 11:2-5.
2. Ni nini Nuhu aliweza kutimiza kwa imani? Urithi gani wa kiroho ulikuwa wake kutokana na tendo hili? Waebrania 11:7.

   **Dokezo**: Kwetu tendo hili laweza kuonekana rahisi. Lakini watu wa siku hizo hawakuwahi kuona mvua mbeleeni na kwa kawaida hawangeweza kuamini jambo hili la mvua kwamba itaiharibu dunia. Nuhu alimwamini Elohim bila ya kujali jinsi jambo hilo lingewezekana. Kwa hivyo lazima tuwe na imani sawa kama hiyo kwa Muumba wetu, kumwamini kikamilifu, kupitia uzoefu wetu wote wa maisha yetu ya sasa.

3. Jinsi gani imani ya Abrahamu ina manufaa kwa mataifa ya ulimwengu? Warumi 4:11-13.
4. Kwa nini tajiriba ya Ibrahimu iliandikwa? Warumi 4:23, 24.
5. Ni ahadi gani ya Elohim inatimizwa sasa katika tendo hili? Mwanzo 17:5-8.
6. Jinsi gani Mtume Paulo anatafsiri neno "uzao"? Wagalatia 3:16.
7. Kama Ibrahimu, jinsi gani tutakubali ahadi za Elohim? Warumi 4:21; Waebrania 11:6.
8. Ni kwa msingi gani imani ambayo itaokoa lazima ijengwe? Warumi 10:17.

9. Ikiwa tutasikia neno na kukosa kutenda kulingana na hilo neno, tumefananishwa na nini? Yakobo 1:22-24.
10. Ni siri gani katika kupokea baraka za Elohim, ambayo sisi sote tunapaswa kutamani katika utendaji wa kazi yetu katika dunia hii? Yakobo 1:25.

******************************

**Somo La Tarehe Desemba 3, 2016.**

**MKUBWA MIONGONI MWENU NI MTUMISHI**

**Somo Kuu: Luka 9:46-62.**

**Fungu La Kukariri: Mathayo 20:27.**

1. Ni ugomvi upi uliotokea miongoni mwa Mitume katika Luka 22:24?
2. Mwokozi alikuwa wa kuhudumiwa au nikuwahudumia wengine? Luka 22:27.
3. Mwokozi alisema nini kuhusu viongozi wa Mataifa kutawala kwa nguvu na kuonyesha mamlaka yao? Marko 10:42.
4. Je, alipendekeza hilo jambo au alililaani katika miongoni mwa viongozi wa Kanisa? Marko 10:43.
5. Mwokozi alitupea mfano wa kuhudumiwa, au kuwahudumia wengine? Marko 10:44, 45.
6. Je, aliwaamuru viongozi na watu wengine wamfuate Yeye, na kuzifuata nyayo zake? Yohana 8:12; 1 Petro 2:21.
7. Ni amri zipi zaidi ambazo zimepeanwa kwa wazee na viongozi kuhusu kulazimisha na uongozi wa nguvu na kwa njia ya kutia watu uoga? 1 Petro 5:1-3.
8. Je, ni nafasi na wajibu upi kwa viongozi katika ulezi wa Kanisa la Elohim? Matendo 20: 28.
9. Ni nini itakuwa kazi ya kila mwanafunzi (mfuasi) wa Masihi kuthibitisha upendo wake kwa ajili yake? Yohana 21:15.

   **Dokezo**: Maneno ya kila mwanafunzi wa kweli yatakuwa yameimarika kwa chakula cha kutia nguvu ili kuweza kukaza mwendo. Pia ataweza kuuondoa ubinafsi kwa njia ya kujikana na kuwapendelea wengine badala yake mwenyewe.

10. Ili kulivutia jukumu hili takatifu juu yetu, Mwokozi wetu alitumia maneno "Kulisha kondoo wangu"; maneno haya yalirudiwa kwa Petro? Yohana 21:16, 17.
11. Je, maisha ya Paulo yalikuwa yamejaa kujikana na dhiki, au yeye (kwa sababu alikuwa kiongozi aliyeteuliwa katika Kanisa la Elohim) alitafuta vitu za kumnufaisha na kufuata maisha ya raha? 2 Wakorintho 11:26-28.
12. Je, Paulo aliwatawala watu kwa vitisho, kuwalazimisha na kuwatia hofu, au walikuwa chiniya amri zake kupitia upendo? Matendo 20:31-35.
13. Je, tumeamriwa kufuata mfano uliowekwa naye Paulo, vile vile kufuata nyayo zake Masihi? 1Wakorintho 11:1.
14. Tunapaswa kutafuta kibali na ushirika wa wale wanaonekana kuwa wakubwa miongoni mwa watu? Warumi 12:16.
15. Ni maelekezo gani mazuri yaliotolewa katika Warumi 12:10?

16. Ni ushuhuda gani tunao katika Waebrania 3:5 kuhusu kiongozi mkuu, aliyechaguliwa na Elohim, katika nyakati za Agano la kale?
17. Ni sifa gani zinazohitajika kwa mtumishi ambazo zimewekwa katika 2 Timotheo 2:24, 25.

******************************

**Somo La Tarehe Desemba 10, 2016.**

**MASIHI NJIA YA UZIMA**

**Somo Kuu: Yohana 14:1-21**

**Fungu La Kukariri: Yohana 14:6**

1. Je, Masihi amejitangaza mwenyewe kuwa nani? Yohana 14:6.
2. Kipawa cha Elohim ni kipi, jinsi gani chapatikana? Warumi 6:23.
3. Ni wangapi wanaweza kufanywa kuwa washiriki wa kipawa hiki? Ufunuo 22:17.
4. Ni nini tunamiliki kama kweli tumemkubali Masihi Yahshua? 1 Yohana 5:12; Yohana 3:16.
5. Ili tuweze kukaa ndani ya Masihi, nini mtu anafaa kufanya? 1 Yohana 2:6; Luka 8:21.
6. Ni ahadi gani Masihi aliweka kwa wale watakaomfuata? Yohana 1:4, 9; 8:12.
7. Wakati mtu anafuata maagizo ya Masihi, ni maisha ya nani yatakaodhihirishwa kwake? Wagalatia 2:20; 2 Wakorintho 5:15.
8. Jinsi gani tunakuwa watoto wa Elohim? Wagalatia 3:26, 27; Wakolosai 2:12; Yohana 3:3.
9. Tunawezaje kuonyesha imani katika Masihi? Yakobo 2:18.
10. Ni kupitia nani wana wa Elohim watakuwa warithi pamoja? Warumi 8:17.
11. Ni kupitia kwa nani wana wa Ibrahimu watapokea ahadi ya urithi wa baadaye? Wagalatia 3:16, 29.
12. Ni kwa nani pekee yake tutapata wokovu? Matendo ya Mitume 4:12; Yohana 10:7, 9.

    **Dokezo**: "Giza litafunika dunia na giza kuu lifunike watu: lakini Bwana atakuzukia wewe, na utukufu wake utaonekana juu yako." Isaya 60: 2.

******************************

**Somo La Tarehe Desemba 17, 2016.**

**MAANA YA KIFO NA KUFUFUKA KWAKE YAHSHUA KWETU SISI**

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:1-23**

**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:22, 23.**

1. Je, ni sababu gani Isaya alitoa kwa ajili ya unabii wa kifo cha Masihi? Isaya 53: 8.
2. Je, Kifo cha Masihi Mwana, kiliamriwa na Elohim Baba? Isaya 53: 6, 10.
3. Je, mwana wa Elohim alijitolea, au yeye alilazimishwa kufa? Mathayo 26:53; Yohana 10:17, 18.

4. Je, Masihi alitabiri kifo na kufufuka kwake mwenyewe? Mathayo 20:18, 19, 16:21-23.
5. Basi Masihi alifanywa kuwa nani? Waebrania 5:8, 9.
6. Jinsi gani tunafaa kukumbuka kifo cha Yahshua? 1 Wakorintho 11:26-32.
7. Yahshua alitabiri nini kuhusu kufufuka kwake? Yohana 2:19-22; Marko 9:31.
8. Kwa nini maisha, kifo na kufufuka kwa Masihi Yahshua, mwana wa Elohim, kuhitajike? (a) ili kutimiza maandiko: Luka 24:44-46; (b) kwa ajili ya msamaha wa dhambi:1 Wakorintho 15:17; (c) kwa ajili ya kuhesabiwa haki: Warumi 4:25; (d) ili kufanya maombezi: Warumi 8:34; Waebrania 9:24.
9. Ni matendo gani yanaashiria kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Masihi? Warumi 6:3-6.
10. Jinsi gani Masihi alijidhihirisha kwa Yohana katika kisiwa cha Patimo? Ufunuo 1:17, 18.

******************************

**Somo La Tarehe Desemba 24, 2016.**

**YAHSHUA AWATOKELEZEA WANAFUNZI WAKE BILA KUTARAJIWA**

Yahshua yu nasi kila siku. Hatupaswi kumtafuta siku ya Sabato tu, katika mikutano ya maombi au nyakati za kimya tunapokuwa naye pekee yetu. Ingawa ni kweli kabisa ya kwamba tunabarikiwa sana na uwepo wake katika nyakati hizo, pia ni kweli ya kwamba, mara nyingi kuliko itupasavyo, tunaye kando katika benchi ya kazi, katika ofisi, wakati sisi tunaosha vyombo, kuendesha gari au shughuli yoyote ya kila siku tunayoshiriki katika. Hizo ni nyakati ambazo tunaweza kosa kumtarajia, na isiwe hivyo. Kazi yetu lazima iwe ya kupendeza kwa Bwana, ili kazi yetu iweze kubarikiwa naye.

**Somo Kuu: Marko 16:9-20**

**Fungu La Kukariri: Yohana 15:16.**

1. Ni amri gani Yahshua aliwapa wanafunzi wake kuhusu kuhubiri neno? Marko 16:16; Mathayo 28: 19; Matendo 1: 8.
2. Kabla ya Bwana Yahshua hajapaa kwenda mbinguni, ni wapi wanafunzi wake walikuwa wamekusanyika? Yohana 21:2, 3.
3. Ni nini inathibitisha kwamba Bwana hakupendezwa na kile walichokuwa wakifanya? Yohana 21:3, sehemu ya mwisho.
4. Ni nani ambaye alionekana ufuoni? Yohana 21:4.
5. Nini kilitendeka wakati walitii amri ya Bwana? Yohana 21:6.
6. Inawezekana kwetu kutimiza chochote bila yeye? Yohana 15:5.
7. Ni swali gani la kutafakari Yahshua aliuliza Petro? Yohana 21:15.
8. Jinsi gani Petro alihisi wakati Bwana alimuuliza mara ya tatu kama kweli alimpenda? Yohana 21:17.
9. Wakati Petro aliona mwanafunzi ambaye Bwana alimpenda akimfuata, ni jambo gani alimuuliza Bwana? Yohana 21:20, 21.

******************************

**Somo La Tarehe Desemba 31, 2016.**

**WOKOVU**

**Somo Kuu: 2 Timotheo 2**

**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 2:15.**

1. Je, mwenye dhambi ana njia moja tu ya kuepuka dhambi na adhabu yake? Matendo 4: 12.
2. Jinsi gani Masihi Yahshua anaweza kuwa wokovu wa mwanadamu kutoka katika dhambi? Wafilipi 2:6-9.
3. Ni toleo gani la ajabu Baba alimpa kila binadamu? Warumi 3:23-26; 5:15-21.

   **Dokezo**: Mtu hawezi kununua wokovu, wala hawezi kujitafutia, kwani ni zawadi ya bure ya mbinguni. Kwa kutumia muda wake mbele ya kiti cha enzi cha mbinguni kwa moyo na akili inayofikilia mambo ya juu pekee yaliyo matakatifu, kuyatamani kwa dhati, na kutafuta na kuyaomba hayo mambo, ni hakika kuyapata. Luka 11:11-13.

4. Jinsi gani tutapata imani inayohitajika kuamini katika mambo haya na kuyatafuta? Warumi10:17.
5. Tukisoma kwa dhati na kujifunza neno lililoandikwa, ambalo lilikuja kwetu kupitia kuongozwa kwa manabii watakatifu, ni nini itafanyika? Isaya 30:21; Warumi 10:8.
6. Je, hatua inayofuata ni nini? Matendo ya Mitume 3:19; 2 Wakorintho 7:10.
7. Ni kwa nani tunafaa kutubu dhambi zetu? Zaburi 32: 5; 1 Yohana 1:9.
8. Tutajua aje kwamba mtu aliyekuwa katika dhambi, ametubu na kugeuzwa katika njia na mwenendo mpya? Mathayo 3:8; Warumi 8:13.
9. Je, tutapata amani ya akili, na dhamiri zetu zitakuwa huru kutokana na hatia, baada ya hatua sahihi kuchukuliwa? Warumi 8:1.
10. Mtu ambaye amezaliwa tena atakuwa akiishi kwa ajili yake mwenyewe tu, au kwa wengine? Atakuwa mtumishi ambaye ana faida kwa Bwana, kwa kusaidia kupeleka ujumbe wa wokovu? Yohana 15:1, 2; Mathayo 25: 29, 30.

*******************************